Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki iwe shauku

Toleo Na. 007 | Jarida la kila miezi mitatu | Julai - Septemba, 2011

# Dk. Shein Ateua Kadhi Mkuu na Mufti Zanzibar

**RAIS** wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein amemteua Sheikh Khamis Haji kuwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar.

Nafasi ya Kadhi Mkuu wa Zanzibar ilikuwa wazi kwa muda mrefu kufuatia aliyekuwa akishika wadhifa huo, Sheikh Ali Khatib Mranzi kufariki.

Kabla ya uteuzi huo uliofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Sheikh Khamis Haji alikuwa Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar.

Afisi ya Kadhi Mkuu wa Zanzibar inasimamia Mahkama zote za Kadhi Zanzibar na Kadhi Mkuu anakuwa Kadhi wa Rufaa wa kesi zilizoanzia Mahkama za Kadhi wa Wilaya.

Sambamba na uteuzi huo, Rais wa Zanzibar aliwateua Makadhi wa Wilaya na Maulamaa wanaokaa na Jaji wa Mahkama Kuu kusikiliza rufaa ya kesi zilizotoka kwa Kadhi wa Rufaa. Mahkama za Kadhi Zanzibar zimeanzishwa chini ya Sheria ya Kadhi Nam. 3 ya 1985.

Uamuzi wa Mahkama Kuu wa mambo ya Kiislamu unakuwa wa mwisho na hauwezi kukatiwa rufaa katika Mahkama ya rufaani ya Tanzania.

Vile vile, Rais wa Zanzibar amemteua Sheikh Saleh Kabi kuwa Mufti wa wa Zanzibar. Aliyekuwa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Harith Bin Khelef alifariki dunia Agosti 26, 2010.

Afisi ya Mufti Zanzibar imeundwa chini ya Sheria ya Afisi ya Mufti Nam. 9 ya 2001 ambayo miongoni mwa kazi zake ni kusimamia mambo ya waislamu na kutoa fatwa.

Katika Jarida la *"Sheria na Haki"* linalochapishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) katika toleo Nam. 006 April-Juni lilichapisha habari za Taasisi Muhimu Tanzania kuwa na ombwe la viongozi.



*Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein*



*Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mheshimiwa Omar Makungu (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya makadhi wapya baada ya kuwaapisha.*

## YALIYOMO

Taarifa Uk. 4

Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Uk. 6

Sheria ya Mirathi ya Zanzibar Uk. 8

Picha za ajali ya M.V Spice Islander Uk.12

Sheria inayolinda zao la karafuu Zanzibar Uk. 18

# Bodi ya Wahariri

**Mhariri:** Prof. Chris Maina Peter

**Msaidizi Mhariri:** Iss-haq I Shariff

**Mwenyekiti:** Harusi M. Mpatani

**Wajumbe:**
Ali Uki
Safia M. Khamis
**Msanifu:**
Yussuf A. Hassan

Ifanye haki

Iwe shauku

*Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:*
***Simu:*** *0242233784*
***P.O.Box:*** *3360 Zanzibar*
***Fax:*** *0242234495*
***E-mail:*** *zlsc@hudumazasheria.or.tz*
***website:*** *www.hudumazasheria.or.tz*

**Wananchi wote mnaombwa kusoma Jarida hili la Kituo kwa madhumuni ya kujifunza zaidi na kupima maendeleo ya utendaji kazi za Kituo. Tunakaribisha barua za maoni kutoka kwa wasomaji na michango ya makala kwa ajili ya kuelimisha umma. Aidha wote watakaopenda kuchangia au kuleta maoni yao katika Jarida la Sheria na Haki wanatakiwa wajitambulishe kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwazi katika kuendeleza Jarida hili. Bodi ya Wahariri itakuwa na uwezo wa mwisho wa kuamua au kuhariri habari itakayochapishwa kwenye Jarida hili.Mhariri.**

## Maoni ya Mhariri

# Ajali ya '*Spice Islanders*' wahusika wawajibike na wawajibishwe kisheria



**Mnamo tarehe 10 Septemba, 2011 wakati wa usiku wa manane meli ya *M.V Spice Islander* iliokuwa ikisafiri kutokea bandari ya Zanzibar kuelekea kisiwani Pemba ilizama katika mkondo mkubwa wa bahari ya Nungwi, Kaskazini Unguja. Watu zaidi ya 200 walipoteza maisha wengi wao wakiwa wanawake na watoto wadogo. Baadhi ya abiria waliokuwemo ndani ya meli hiyo walipotea moja kwa moja na hata miili yao haijapatikana hadi leo.**

**Hii ilikuwa ajali ya kutisha na kushtua sana kwa Wazanzibari, Watanzania na jamii ya kimataifa. Kinachouma zaidi ni kwamba taarifa zote zinazopatikana hadi leo zinaashiria kuwepo kwa uzembe mkubwa kuwa chanzo cha ajali hii. Meli ilikuwa imebeba mizigo mingi na mizito kupita kipimo kinachoruhusiwa kisheria na pia abiria wengi na ambao hata idadi yao haijulikani. Ilimradi sheria zote zilikuwa zimekiukwa. Huu ni utaratibu ambao haukubaliki kabisa.**

**Matokeo yake ni kwamba watu wasio na hatia wamepoteza maisha yao. Katiba ya Zanzibar ya 1984 inaainisha vizuri haki ya kuishi kwa kila Mzanzibari. Kifungu cha 13 (1) cha Katiba kinasema kwamba *"kila mtu anayo haki ya kuwa na hifadhi ya maisha yake."* Jukumu la kulinda maisha ya Wazanzibar lipo mikononi mwa Serikali. Hivyo, Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba wananchi wanasafiri kwa usalama, kwa vyombo vyenye uwezo wa kufanya kazi yake na vilivyosajiliwa na kufuata sheria zote husika za Zanzibar.**

**Bila kutaka kutonesha kidonda, inabidi kukumbusha kwamba hii siyo ajali ya kwanza inayohusu vyombo vya baharini hapa Zanzibar. Mara nyingi pamekuwa na taarifa nyingi za Boti za abiria kuzima katikati ya bahari na kuwaletea abiria fadhaa kubwa. Miaka michache iliyopita meli ya abiria ya *M.V Fatih* ilizama katika bandari ya Malindi, Unguja. Iliundwa Tume iliyoongozwa na aliyekuwa Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar, Mhe. Omar Makungu (sasa Jaji Mkuu wa Zanzibar) kuchunguza ajali hiyo na ripoti yake kutolewa. Katika mazingira ya kawaida, watendaji wa mamlaka husika wangelijifunza ili kuepusha ajali. Kinyume yake inaonekana ripoti ya Jaji Makungu imewekwa kabatini na uzembe unaendelea *(business as usual).***

**Tunafahamu kwamba Tume ya Uchunguzi wa ajali hii ya sasa ya *M.V Spice Islander* imeteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein na sasa inafanya kazi. Lakini kuundwa kwa Tume hakutunyimi haki yetu ya uhuru wa maoni iliyoelezwa katika Kifungu cha 18 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.**

**Upande wetu tumeshangazwa na baadhi ya mambo yaliofanyika kuhusiana na ajali hii. Kwanza, haieleweki kwa nini mashtaka ya jinai dhidi ya wale waliohusika moja kwa moja na ajali hii yamesimamishwa na hali Tume na kesi ni vitu viwili tofauti kabisa. Pili, hadi sasa wananchi hajawapewa taarifa ya wazi kuhusu umiliki wa chombo hiki. Kumekuwa na kujikanyaga kwingi kuhusu suala hili. Tatu, katika kufuata dhana ya uwajibikaji katika utawala ilitegemewa kwamba Waziri mwenye dhamana ya usafiri angekuwa tayari ameachia ngazi na kujiuzulu kwa kuheshimu dhana hii ya (*Ministerial Responsibility*). Uwajibikaji wa Waziri lakini hadi sasa bado ameng'ang'ania ofisini wakati uchunguzi ukiendelea dhidi ya ofisi yake. Nne, baadhi wa wajumbe wa Tume wanahusika moja kwa moja na mamlaka zinazohusika na usafiri wa meli na hivyo kukosa kabisa sifa za kuwa wajumbe katika Tume hii ya Rais kwa sababu ya mgongano wa maslahi (*conflict of interest)* na hivyo kuwepo kwa uwezekano wa wao kushindwa kutenda haki au kuonekana kwamba wametenda haki.**

**Haya mambo tulioyaeleza hapo juu huenda yakaitia dosari Ripoti itakayotokana na Tume ya Mhe. Rais na hii haitatoa picha nzuri kwa nchi yetu. Kwa sasa tunachoweza kusema ni kumuomba Mhe. Rais na viongozi wenzake wawe wakali. Panapotokea uzembe wa aina yoyote ile waruhusu sheria ichukuwe mkondo wake moja kwa moja. Kwa Wazanzibari, tunashauri kwamba cha muhimu ni kujenga utamaduni wa kuheshimu na kufuata sheria wakati wote. Tukifanya hivyo, mambo kama haya ya *M.V Spice Islander* yatakuwa historia.**

***Prof. Chris Maina Peter***
***Mhariri.***







***Jengo la Tume ya Haki za Binadamu, Dar es Salaam.***

# Kikwete Atangaza Viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu

**MAKAMISHNA** wa TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania wametangazwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Rais Kikwete alimtangaza Mwenyekiti na Makamishna wa Tume hiyo baada ya kipindi kirefu Tume kutokuwa na viongozi na kusababisha malalamiko ya ufuatiliaji wa haki za raia na utoaji wa maamuzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa katika tovuti ya Tanganyika Law Society Secretariat, Rais Kikwete alimteua tena Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna waliokuwa katika Tume hiyo kabla ya kumaliza muda wao.

Walioteuliwa ni Mwenyekiti Mheshimiwa Jaji mstaafu Hamis Maneto na Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Mahfoudha A. Hamid.

Wengine walioteuliwa ni Kamishna Joaquine Demello, Kamishna Zahor J. Khamis, Kamishna Bernadeta Gambishi, Msaidizi Kamishna Constanti Mugusi na Msaidizi Kamishna Fahamu Mtulya.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Miongoni mwa majukumu ya Tume ni kuhamasisha hifadhi ya Haki za Binadamu, kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa Haki za Binadamu kwa jumla na kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora.

Jarida la Sheria na Haki linalochapishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) katika tolea Nam. 006 April-Juni 2011 lilichapisha habari ya Taasisi Muhimu kuwa na pengo la viongozi.



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete.***

TRANSFORM JUSTICE INTO PASSION

**ZANZIBAR LEGAL SERVICES CENTRE (ZLSC)**

House No. 37 Migombani (Opposite Migoz Supermarket)
Box 3360 Tel (024) 2233784 Fax (024) 2234495
E-Mail: zlsc@hudumazasheria.or.tz
Website: hudumazasheria.or.tz
Zanzibar – Tanzania

Sub-Office: Chake Chake, Pemba Tel: (024) 2452936

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI MAOMBOLEZO AJALI YA MELI YA M.V. SPICE ISLANDER

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo ya zaidi ya watu 200 wakiwemo watoto wadogo kufuatia kuzama kwa meli ya ***M.V. Spice Islander*** katika mkondo wa Bahari ya Nungwi uliopo eneo la Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja wakati wa usiku wa manane. Meli hiyo ilikuwa ikitoka Bandari ya Malindi, Zanzibar na kuelekea kisiwa cha Pemba.

Kwa niaba ya ***Bodi ya Wadhamini na Uongozi na Wafanyakazi wote Kituo cha Huduma za Sheria*** **Zanzibar** kinatoa mkono wa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki , Wazanzibari na Watanzania wote kwa msiba mzito uliotufika. Tunawaombea Dua na malazi mema peponi wote waliofariki katika ajali hiyo na tunawapa pole kwa wale walionusurika.

Aidha, Kituo kinampongeza Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Viongozi wengine kwa kushiriki moja kwa moja katika shughuli za uokoaji hadi mazishi ya Marehemu wa ajali hii mbaya. Vile vile Kituo kinafarijika na ushikiano wa dhati ulioonyeshwa na taasisi zote za Serikali na zisizokuwa za Serikali; na watu binafsi katika shughuli zote zilizohusika katika msiba huu mkubwa wa kitaifa.

**Hata hivyo,** Kituo kinalazimika kutoa kauli kali kutokana na kukatishwa kwa **haki ya msingi ya kuishi ya watu hao kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 13 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinachosema kwamba *"kila mtu anayo haki ya kuwa na hiafadhi ya maisha yake"* na 13 (2) *kinachosema kwamba "kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hiafadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria."***

Tunaamini kwamba ajali hiyo imesababishwa kwa njia moja au nyingine **uzembe mkubwa** *na* **kutoheshimu sheria** kwa taasisi husika zinazosimamia usafiri wa Baharini. Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutamka kwamba itaunda Tume ya Kuchunguza Ajali hiyo kubwa. **Katika kuunda Tume hiyo, Kituo kinaomba yafuatayo yazingatiwe:**

**(i) Tume iwe huru na isiingiliwe katika utendaji wa majukumu yake;**
**(ii) Tume ijumuishe wajumbe kutoka nje ya taasisi za Serikali na vyombo vya usalama;**
**(iii) Wajumbe wa Tume waongozwe na maadili ya ukweli na haki bila ya kujali nani aliyehusika na nani ataathirika na Ripoti ya Tume;**
**(iv) Ripoti ya Tume iwekwe wazi na isipunguzwe yaliyomo ndani yake;**
**(v) Watakaobainika wawajibishwe kwa mujibu wa sheria za Utumishi;**
**(vi) Vile vile, watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria;**
**(vii) Tume ijadili na isisitize kujengwa kwa Utamaduni wa kuheshimu sheria na kanuni.**

Kituo kitakuwa tayari kutoa msaada wa kisheria kuhakikisha waliohusika kuvunja sheria za usafiri wa baharini na kusababisha ajali hiyo wanafikishwa Mahkamani na sheria inachukua mkondo wake. Pia Kituo kimejipanga ili kiweze kuwasaidia wale wote waliathirika kwa njia moja au nyingine na ajali hii wapate haki na stahili zao kwa mujibu wa sheria.

Tunawapa pole ndugu, jamaa, marafiki, Wazanzibari na Watanzania wote kwa msiba mzito.

**Prof. Chris Maina Peter**
**MWENYEKITI**
**BODI YA WADHAMINI**
**KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR**

**12 Septemba, 2011**



# Huduma za Polisi Tanzania

**Na Fatma Hemed, ZLSC Unguja**

**UTANGULIZI.**

**JESHI** la Polisi Tanzania ni moja kati ya taasisi za ulinzi ya Muungano inayopaswa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao. Huduma zinazotolewa na Jeshi la Polisi zinafuata Waraka Nam. 2//2009 wa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP).Makala hii inaeleza huduma zinazotakiwa kutolewa na Jeshi la Polisi kwa wananchi.

**MAANA YA HUDUMA ZA POLISI.**

Huduma za Polisi ni ushauri au maelekezo yanayotolewa na Afisa wa Polisi kwa Mteja ambaye atahitaji msaada wa Polisi kwa ajili ya kutafuta utatuzi wa kisheria juu ya jambo ambalo limemfika. Kawaida Jeshi la Polisi hutoa huduma au maelekezo ya matukio yanayohusiana na Sheria za Jinai.

Huduma za Polisi kwa mteja hutolewa kwa kuzingatia ubora kutokana na Sheria ndogo zinazoweka utaratibu wa utendaji wa kazi za Polisi *(Police General Orders)* au PGO 107 inasisitiza kwamba mteja atakayefika katika Kituo cha Polisi mambo yafuatayo lazima yazingatiwe;-

1. Mteja asipuuzwe na kudharauliwa.
2. Mteja ahudumiwe kwa haraka na umakini.

**TARATIBU ZA KUMJALI MTEJA.**

Kanuni za Utendaji wa Jeshi la Polisi (PGO 107) zinamtaka Afisa wa Jeshi la Polisi kuzifuata, taratibu hizo kama zifuatazo:-

a) Kujitambulisha. Polisi yeyote ambaye atakuwa na dhamana ya kutoa huduma kwa mteja ni lazima kwanza ajitambulishe jina lake, cheo chake na kituo ambacho anafanyia kazi zake. Hii itaondoa hofu na kujenga ukaribu zaidi baina ya Afisa wa Polisi na mteja.
b) Kumsikiliza tatizo lake kwa makini. Afisa atakayetoa huduma ahakikishe anasikiliza kwa makini. Taarifa za mteja ziandikwe katika buku la kumbukumbu (RB- Report Book) na kuzifanyia kazi. Ikiwa kutahitajika kukamatwa kwa mtuhumiwa, ni jukumu la Polisi kuandaa utaratibu.
c) Utumiaji wa lugha. Afisa wa Polisi atumie lugha safi ambayo itarahisisha mawasiliano baina ya yeye na .
d) Maelezo ya mashahidi yachukuliwe haraka bila ya kucheleweshwa na iwe katika muda waliopangiwa. Ni wajibu wa Polisi kuhakikisha wananchi wanatendewa kwa ukarimu, uwazi na kulingana na sheria.

**MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUTOA HUDUMA BORA KWA MTEJA.**

a) Ajue wateja na tabia zao.
b) Tatizo husika linahusiana na sheria ya jinai au madai.
c) Asiegemee upande wowote.
d) Asitoe hukumu juu ya lalamiko analolishughulikia na aiachie Mahkama.

**POLISI KUSHINDWA KUTEKELEZA TARATIBU HIZI ATAKUWA AMEFANYA KOSA**

Kutokana na Kanuni za Utendaji wa Jeshi la Polisi (PGO) 107 inaeleza kwamba *"Maofisa ambao watadhalilisha ama watapinga mamlaka haya watakuwa wametenda kosa na watawajibika kufukuzwa kazi".* Hii ni kwa mujibu wa Peo ya 6 ya Kanuni za Utendaji wa Jeshi la Polisi (PGO 107).

**FAIDA ZA KUMJALI MTEJA**

Baadhi ya faida za kumjali mteja.

i. Wateja watafurahia na kulipenda Jeshi la Polisi kutokana na huduma bora wanazozipata.
ii. Kupata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wananchi hasa katika taarifa za matukio ya uhalifu yaliyotokea au yanayotaka kutendeka.
iii. Jeshi la Polisi litaweza kupambana na uhalifu kwa mafanikio kutokana na jamii kuwa na imani nao.

**CHANGAMOTO.**

Polisi wanakumbana na changamoto mbalimbali, mfano ni :-

i. Vitendea kazi.
ii. Upungufu wa Askari
iii. Ukosefu wa usafiri katika Vituo vya Polisi.
iv. Uwezo mdogo wa kumudu kazi.
v. Polisi kujifanya wasuluhishi wa mizozo zaidi. Mfano kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kutilisha saini mikataba ya malipo ya pesa ndani ya Vituo vya Polisi.
vi. Lugha chafu kwa wateja.
vii. Wateja kusubiri muda mrefu kupatiwa huduma.

**MAPENDEKEZO.**

Ili huduma bora kwa mteja ziwe nzuri na za kuridhisha mapendekezo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:-

1) Elimu ya kutosha itolewe kwa Maafisa wa Polisi ili kuepusha suala la kufanya kazi ambazo kisheria hawapaswi kuzifanya.
2) Vitendea kazi viongezwe katika Vituo vya Polisi ili kuweza kurahisisha kukamatwa kwa wahalifu mara tu matukio yanaporipotiwa katika Vituo hivyo.
3) Maafisa wa Jeshi la Polisi wawe tayari kufanya kazi kwa kuzingatia taratibu za kazi zinavyoelekeza ili kuepusha utumiaji mbaya wa lugha kwa wateja wanaowahudumia.
4) Wateja wahudumiwe kwa wakati ili kuepusha msongamano wa watu katika Vituo ya Polisi.

**HITIMISHO.**

Suala la kuwahudumia wateja ndani ya Jeshi la Polisi linahitaji kupewa kipaumbele kikubwa hasa ukizingatia kuwa wananchi walio wengi wanaamini kuwa endapo utapatwa na tatizo la uvunjwaji wa sheria; Polisi ndio sehemu ya kwanza kuripoti lalamiko lako ili hatua za kisheria kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kufunguliwa Mashtaka. Ni jukumu la Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa kipaumbele katika kupatiwa huduma bora iliyo bora.

# Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi

Na Safia Sultan, ZLSC Pemba

**UTANGULIZI:**

**SHERIA** ya Fidia ya Wafanyakazi Nam. 5 ya 2005 imetungwa kwa ajili ya kuwafidia wafanyakazi ambao wamepata madhara wakiwa kazini. Sheria hii imekuja kufuta Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi ya 1986 na kuweka masharti bora kwa ajili ya kuwafidia wafanyakazi ambao wataumia wakiwa kazini.

Kwa mujibu wa makala hii, Sheria inamaanisha ni Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi.

**MAANA YA MUAJIRI NA MFANYAKAZI**

**MUAJIRI**: Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Nam. 5 ya 2005, muajiri maana yake ni mtu aliyeajiri au anayetoa kazi kwa mtu yoyote na kumlipa mtu huyo au kuahidi kumlipa.

**MFANYAKAZI**: Kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Nam. 5 ya 2005 mfanyakazi maana yake ni mtu ambae:

a) Ameajiriwa au anaefanyakazi kwa muajiri na ambae analipwa au anastahiki kulipwa malipo kwa kazi hiyo
b) Anafanyakazi chini ya uongozi au uangalizi wa muajiri au wa mtu mwengine.
c) Ni mfanyakazi anayejifunza kazi.

**DHIMA YA MUAJIRI**

Muajiri ni kiunganishi kikubwa baina ya mfanyakazi na ajira yenyewe. Hivyo Muajiri anakuwa na dhima kwa mfanyakazi wake ili kuhakikisha ufanisi wa ajira hio.

Dhima ya muajiri imezungumzwa katika Kifungu cha 4(i) ambapo muajiri atakuwa na dhima ya kumlipa mfanyakazi fidia iwapo mfanyakazi huyo amepata majeraha ya mwili ambayo yamesababishwa na ajali inayotokana na kazi au ndani ya kazi ya muajiri.

Hata hivyo muajiri hatokuwa na dhima kwa mfanyakazi chini ya Kifungu cha 4 (a na b) ikiwa mfanyakazi atapata majeraha kwa kipindi cha chini ya siku tatu mfululizo hataweza kupata malipo katika kazi ambayo ameajiriwa, au ikithibitika kwamba majeraha ya mfanyakazi yanatokana na vitendo vibaya na vya makusudi vya mfanyakazi isipokuwa ikiwa majeraha hayo yatapelekea kifo au majeraha mabaya ya kutia ulemavu wa kudumu. Katika hali hii Mahkama kwa kuzingatia mazingira yote inaweza kutoa fidia iliyowekwa kwenye sheria hii au sehemu ya fidia kama itakavyoona inafaa.

Ulemavu wa kudumu umetafsiriwa na sheria hii katika Kifungu cha 3 kuwa ni ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kutofanya kazi yoyote ambayo alikuwa anaweza kuifanya wakati wa ajali



*Wafanyakazi wakitekeleza majukumu yao.*

inayopelekea kupata ulemavu.

Muajiri vile vile kwa mujibu wa kifungu cha 4(3) muajiri atakuwa na dhima kwa mfanyakazi iwapo mfanyakazi amepata majeraha kutokana na ajali inayotokea wakati mfanyakazi anakwenda au anarudi moja kwa moja kazini. Majeraha haya yatahesabiwa kuwa ni maumivu aliyopata akiwa kazini. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (4) itakuwa ni jukumu la mfanyakazi aliyepata maumivu kutokana na ajali wakati akienda au kurudi kazini kuonesha kwamba alipita njia ya moja kwa moja.

Kwa mujibu wa sheria hii, ajali yoyote ile itakayopelekea kifo au majereha mabaya ya ulemavu wa kudumu yatachukuliwa yanatokana na ajira, bila ya kujali kwamba mfanyakazi kwa wakati huo alikuwa akivunja taratibu za kazi, lakini kitendo hicho kiwe kimefanywa na mfanyakazi kwa madhumuni ya au kuhusiana na biashara au kazi ya muajiri. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 4A, lakini kwa mujibu wa Kifungu cha 4B hapana fidia yoyote atakayopewa mfanyakazi ikiwa amepata ulemavu wa kudumu au kifo kinachotokana na majeraha ya kujitakia kwa makusudi.

**FIDIA YA MAJERAHA KWA WAFANYAKAZI.**

Fidia ya majeraha imeonyeshwa katika sehemu ya tatu ya sheria hii.

Katika Kifungu cha 10 (1 na 2) cha sheria hii kimeweka wazi endapo mfanyakazi amepata majeraha yanayotokana na ajira yaliyosababisha kifo chake, na ikiwa mfanyakazi huyo ameacha mrithi yoyote, kiwango cha fidia kitakuwa ni jumla sawa na mapato ya miezi thelathini na sita, na gharama za mazishi zisizopungua thuluthi moja ya gharama zote.

Iwapo mfanyakazi amepata ulemavu wa kudumu uliotokana na ajira, kiwango cha fidia kitakuwa jumla ya mapato ya miezi arubaini na nane au shilingi milioni tano, au kiwango chochote kilichokuwa kikubwa. Pia ikiwa majeraha yamesababisha ulemavu wa kudumu kwa kiasi ambacho mfanyakazi aliyeumia anahitaji msaada wa mtu mwengine wakati wote, atalipwa fidia ya ziada inayofikia robo ya kiwango anachotakiwa kulipwa chini ya Kifungu cha 11 (1 na 2) cha sheria hii.

Aidha katika Kifungu cha 12(1) kimemuelezea mfanyakazi ambaye amepata ulemavu wa kudumu usiokuwa kamili ambao umetokana na majeraha, kiwango cha fidia kitakuwa ni asilimia iliyotathminiwa na daktari anayetambulika ya mapato ya miezi arubaini na nane ikiwa ni asilimia ya kukosa mapato iliyosababishwa na majeraha.

Kifungu cha 3 cha Sheria hii kimetoa tafsiri ya ulemavu usio kamili, ulemavu wa muda na ulemavu wa kudumu. Ulemavu usio kamili maana yake ni ulemavu ambao unamzuia kwa kiasi fulani mfanyakazi kutofanya kazi na unaelezwa kwa njia ya asilimia itakayoamuliwa na daktari anayetambulika.

Aidha ulemavu wa muda maana yake ni ulemavu ambao unamzuia na kupunguza uwezo wa kupata kipato wa mfanyakazi katika ajira yoyote ambayo alikuwa akifanya wakati ajali iliyopelekea ulemavu ilipotokea. Na ulemavu wa kudumu maana yake ni ulemavu ambao unamzuia mfanyakazi kutofanya kazi yoyote ambayo alikuwa anaweza

Inaendelea Uk. 5





# Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi

*Inatoka Uk. 4*

kuifanya wakati wa ajali iliyopelekea kupata ulemavu.

Vile vile katika Kifungu cha 13(1) a na b kimeweka wazi kwa yule mfanyakazi ambaye atapata ulemavu wa muda ikiwa ni kamili au usio kamili lakini umetokana na majeraha aliyoyapata katika ajira, fidia yake itakuwa ni malipo ya vipindi yatakayolipwa kama itakavyokubaliwa au mahakama itakavyoamrisha au malipo ya jumla yaliyofanyiwa hesabu kwa kuangalia muda wa ulemavu, mabadiliko ya ulemavu kwa kukisia.

Malipo hayo ya vipindi yatakuwa malipo ya mwezi ya nusu ya malipo ambayo mfanyakazi alikuwa akipata wakati wa ajali ukitoa malipo anayopata au anayoweza kupata katika ajira inayomfaa baada ya ajali yakiwemo:-

**a.** Muda uliopotea hospitali au aliokuwa hayupo kazini uliothibitishwa na daktari kuwa ni wa lazima. Muda huo utachukuliwa kuwa ni ulemavu wa muda bila ya kuangalia matokeo ya majeraha na muda wowote mwengine wa baadaye kabla ya tathmini ya mwisho ya ulemavu utachukuliwa kuwa ni muda wa ulemavu wa muda usiokuwa kamili. Muda wote huo ukienda sambamba, tofauti ya malipo na kipindi cha juu cha malipo ya vipindi hakitozidi miezi tisini na sita.

**b.** Na endapo kifo kitatokezea au ulemavu wa kudumu baada ya ulemavu wa muda, mkato utafanywa kutoka katika kiwango cha jumla kilicholipwa chini ya Kifungu cha 10 na 11 cha Sheria hii.

**FIDIA NA MAJERAHA KWA WACHUMA KARAFUU.**

Fidia na majeraha kwa wachuma karafuu imeonyeshwa katika sehemu ya IV ya Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Nam. 5 ya 2005

Katika sehemu hii Kifungu cha 15 kimetoa maana ya "mchumaji karafuu" pamoja na "muajiri".

"Mchumaji karafuu" ni mfanyakazi anayepata mshahara wa kima cha chini anayetambuliwa na Serikali na "Muajiri' maana yake ni Serikali ya Zanzibar.

Ikiwa katika uchumaji karafuu, mchumaji karafuu ameumia kutokana na ajali inayotokana na kazi hiyo, muajiri wake atakuwa na dhima ya kulipa fidia. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 16 , lakini Kifungu cha 17(1) kimeeleza iwapo mchumaji karafuu amepata ulemavu wa kipindi cha chini ya siku tatu mfululizo fidia haitolipwa kwa mtu huyo.

Vile vile, hakuna fidia itakayolipwa kwa mfanyakazi ikiwa itathibitika kuwa majeraha aliyopata yanatokana na vitendo vyake vya hatari na vya makusudi isipokuwa kwamba;

- Majeraha hayo yatapelekea kifo au
- Ulemavu wa kudumu endapo majeraha aliyoyapata



*Mfanyabiashara akiuza shokishoki sokoni mjini Unguja.*

mchumaji karafuu yatapelekea mambo hayo mawili yaliyotajwa hapo juu basi Mahkama kwa kuzingatia mazingira yote inaweza kutoa fidia iliyowekwa na sheria hii kama itaona inafaa.Hii imeonyeshwa katika Kifungu cha 17(2).

Kifungu cha 18 kimezungumzia majeraha ya kujitakia mwenyewe, endapo majeraha ya makusudi ya kujitakia mwenyewe yaliyosababisha kifo au ulemavu wa kudumu yamefanywa na mchumaji karafuu basi hakuna fidia itakayolipwa chini ya sheria hii.

**OMBI LA FIDIA**

Ombi la fidia limeelezwa katika Kifungu cha 23(2) ambapo ombi hilo linatakiwa lifanywe ndani ya miezi sita tokea ajali iliyosababisha majeraha ilipotokea, au kwa upande wa kifo kikitokezea basi madai vile vile yawe ndani ya miezi sita tokea kifo kitokezee. Isipokuwa kwamba kushindwa kupeleka ombi ndani ya wakati ulioainishwa haitozuia ufunguaji wa kesi ikiwa itagundulika kwamba kushindwa huko kunatokana na makosa au sababu nyengine ambayo ni ya msingi kisheria

Kifungu cha 24(1-3) kinampa dhima muajiri kuweza kutoa notisi ya ajali ya mfanyakazi, ambayo itapelekwa kwa Mkaguzi wa Afya au Afisa mwengine yoyote ambaye ameruhusiwa na Mkaguzi wa Afya.

Muajiri atalazimika kutoa notisi au ripoti ya ajali iliyosababisha majeraha kwa mfanyakazi ambaye anastahiki kulipwa fidia. Notisi hio itakayotolewa na muajiri itakuwa katika fomu iliyoainishwa kwa Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii au Naibu wake au mtu mwengine yoyote aliyeruhusiwa na yeye. Notisi hio inapaswa kutolewa mapema iwezekanavyo baada ya tukio na kabla mfanyakazi hajaondoka kwa hiari yake katika ajira ambayo amepata majeraha. Hii inaonekana katika kifungu cha 24(1) cha sheria hii. Muajiri akishindwa kufanya hivyo bila ya kuwa na sababu za msingi atakuwa ni mkosa na kosa likithibitika atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi miwili au vyote viwili na hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 24(3).

Kifungu cha 24(2) kinaeleza endapo kifo cha mfanyakazi kilichotokea ndani ya ajira kimetolewa notisi au taarifa imefika kwa muajiri, muajiri mapema iwezekanavyo atoe notisi kwa Mkaguzi wa Afya au Afisa mwengine ambaye ameruhusiwa na Mkaguzi na notisi hio ieleze mazingira ya kifo cha mfanyakazi ikiwa yanaeleweka na muajiri.

Kifungu cha 26(1) kimewapa fursa muajiri na mfanyakazi kukubaliana fidia.

Makubaliano hayo yatakuwa katika sehemu mbili, nakala moja ataiweka muajiri na moja ataiweka mfanyakazi, isipokuwa kwamba:-

a. Fidia itakayokubaliwa isiwe chini ya kiwango kinachotakiwa kulipwa chini ya sheria hii na
b. Endapo mfanyakazi hawezi kusoma na hafahamu lugha ambayo makubaliano yameandikwa, makubaliano hayo hayatambana isipokuwa yawe yamethibitishwa na Cheti cha Mkaguzi wa Afya kwamba amemsomea na kumueleza mfanyakazi masharti yaliyokuwemo na kwamba mfanyakazi ameyafahamu na kuyakubali kwa makubaliano.

Makubaliano hayo yaliyofanywa baina ya mfanyakazi na muajiri yanaweza baada ya kufanyiwa maombi Mahkamani kufanywa amri ya Mahakama. Na hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 26(2).

**CHANGAMOTO.**

1. Wafanyakazi wengi hawaijui sheria hii.
2. Wafanyakazi ambao wanaijua sheria hii, hawajui muda wa ukomo wa kutoa maombi yao ya fidia *(limitation time)*.
3. Utekelezwaji wa sheria hii ni kikwazo.
4. Jumuiya za Wafanyakazi *(trade unions)* zinakosa nguvu ya pamoja kuweza kutetea maslahi ya wafanyakazi.

**HITIMISHO.**

Ili kuweka utawala bora pamoja na kuzingatia maslahi ya nchi na wananchi wenyewe,ni vyema kwa Serikali pamoja na Jumuiya za Wafanyakazi kutilia mkazo utekelezaji wa sheria hii kwani wafanyakazi ndio msingi wa kuleta maendeleo ya nchi.

# Ijue Sheria ya Mirathi ya Zanzibar *(Succession Decree Cap 21)*

**Na Jasadi A. Bungala, ZLSC Unguja**

**UTANGULIZI**

**MIRATHI** ni miongoni mwa mambo yanayoisumbua jamii ya Tanzania na Zanzibar kwa ujumla. Matatizo ya mirathi hutokezea pale mrithiwa anapofariki na kuacha mali nyingi. Migongano kati ya wanafamilia hutokea na kusababisha mifarakano. Makala hii itaelezea ni vitu gani vya kuzingatia wakati wa kurithi mali ya marehemu. Kwa upande wa Sheria za Kiislam watafuata Quraan na Hadithi za Mtume Muhammad (SAW) na wasiokuwa Waislamu watafuata Sheria ya Mirathi Sura ya 21 Sheria za Zanzibar.

Mahkama ya Kadhi imepewa mamlaka ya kisheria chini ya sheria ya Kadhi's Nam. 3 ya 1985 na kwa upande wa wasiokuwa waislam wao wanafuata Sheria ya Mirathi Sura ya 21 ya Sheria za Zanzibar,na ndio sheria tunayoiangalia katika makala hii.




*Wosia wa mirathi*

**MAANA YA MIRATHI.**

Mirathi ni mali aliyoacha marehemu, mali hii hurithiwa na warithi wake halali. kifungu cha 28 ,29,30,31 na 32 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar. Sheria imeweka taratibu maalum zinazoongoza ukusanyaji, uangalizi, usimamizi, ugawaji na umiliki wa mali za marehemu pamoja, na kulipa madeni aliyoacha marehemu wakati wa uhai wake au gharama zitokanazo na mazishi yake. *"Msimamizi wa mirathi anatakiwa akusanye mali za marehemu na madeni aliyokuwa akidai na kulipa madeni aliyokuwa akidaiwa vile vile ni jukumu la msimamizi wa mirathi kutoa fedha kwa ajili ya shughuli za mazishi ya marehemu".*

**MAANA YA WOSIA**

Wosia ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake kuonyesha nia yake jinsi gani angependa mali yake igawanywe baada ya kufa kwake. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar.

**AINA NA SIFA ZA WOSIA**

Wosia unaweza kuwa wa namna mbili; wosia wa mdomo na wosia wa maandishi.

**A) WOSIA WA MAANDISHI LAZIMA:**

Uandikwe kwa kalamu ya wino na sio kalamu ya risasi (inayoweza kufutwa futwa), Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 52 Kifungu kidogo cha 2 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar Sura ya 21 kwa wale wasiokuwa waislam .

- Muusia awe na akili timamu wakati anatoa au anaandika wosia huo, Utaje tarehe ulipoandikwa, Utaje kuwa muusia anayo akili timamu na anausia kwa hiari yake mwenyewe,
- Ushuhudiwe na mashahidi wanaojua kusoma na kuandika angalau wawili (mmoja wa ukoo na mwingine mtu ambaye hahusiki katika mirathi hiyo), kama muusia anajua kusoma na kuandika. hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 52 Kifungu kidogo cha 2 (h) cha Kanuni ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar Sura ya 2 ikisomeka pamoja na Kifungu cha 49 Kifungu kidogo cha 4 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar .
- Ushuhudiwe na mashahidi wasiopungua wanne (wawili wa ukoo na wawili watu baki), kama muusia hajui kusoma na kuandika. hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha Kanuni ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar .
- Wanaotarajia kurithi hawaruhusiwi kushuhudia wosia huo.
- Usainiwe na muusia mbele ya mashahidi wake wakiona, Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 54 cha Kanuni ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar.
- Kutia sahihi yake au kama hajui kusoma, aweke alama ya dole gumba la kulia, hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 52 cha Kanuni ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar.

Utiwe sahihi za mashahidi, Mashahidi wawe wamechaguliwa na muusia mwenyewe. Katika shauri la ***ABDUL SADIKI v. WILFRED RUTAKUNIKWA,*** (1988) High Court of Tanzania at Mwanza TLR 167 Mahkama Kuu ya Tanzania ilitamka kuwa kama muusia hajui kusoma wala kuandika, wosia huo, kulingana na Kanuni ya 19 na 21 ya *Local Customary Law* (*Declaration*) Order, Nambari 4 ya 1963, lazima ushuhudiwe na wanaukoo angalau wanne. Kumbuka: Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria mbali mbali, Sura ya 21, wosia wa maandishi waweza kubadilishwa kwa wosia mwingine wa maandishi unaotaja kubadilisha wosia wa kwanza na unaofuata hatua zile zile kama ilivyoainishwa hapo juu.

**B) WOSIA WA MDOMO LAZIMA:**

- Ushuhudiwe na mashahidi wanne (wawili wa ukoo na wawili watu ambao sio warithi wa mali ya marehemu), Muusia awe na akili timamu , Kama mashahidi watakufa kabla ya muusia kufa, basi wosia hautakubalika na urithi utagawanywa kadri ya mpango wa urithi usio wa wosia.Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 60,61na62 vya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ya Zanzibar Na Kifungu cha 63. Mwenyewe kama anataka kuusia mali zake, atoe wosia mpya, Mashahidi wawe wamechaguliwa na muusia mwenyewe. Katika shauri la ***JOHN NGOMOI v. MOHAMED ALLY BOFU,*** (1988) High Court of Tanzania at Dar es Salaam TLR, 63 Mahakama Kuu ya Tanzania ilitamka kuwa lengo la sharti kwamba angalau nusu ya mashahidi wa wosia wa marehemu lazima wawe wanandugu, ni kulinda usalama wa mali za marehemu dhidi ya udanganyifu, kwani wosia uliozungukwa na mazingira ya udanganyifu ni batili.

**MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUOMBA USIMAMIZI WA MIRATHI MAHAKAMANI.**

1. Uwezo wa mahkama kisheria

Madai yote yanayohusiana na mirathi lazima yapelekwe katika Mahkama yenye uwezo kisheria. Kwa mujibu wa sheria ya mirathi ya Zanzibar Mahkama Kuu ndio iliyopewa uwezo huo na msajili wa Mahkama za Wilaya kwa Pemba.

2. Kama kuna wosia wa marehemu

1. Msimamizi wa mirathi aende akafungue mirathi Mahkamani akiwa na
a) Wosia uliachwa na marehemu.
b) Cheti cha kuthibitisha kifo cha marehemu.
2. Mahkama kutoa tangazo la maombi ya kuteuliwa msimamizi wa mirathi kwa muda wa siku 90, lengo la tangazo

*Inaendelea Uk. 9*





# Ijue Sheria ya Mirathi ya Zanzibar *(Succession Decree Cap 21)*

*Inatoka Uk. 8*

ni kwamba kama mtu yeyote ana pingamizi dhidi ya wosia au msimamizi wa mirathi basi awasilishe mahkamani. Kama hakuna tatizo lolote msimamizi hukabidhiwa barua ya kuhalalisha uteuzi wake na majukumu yake.

3. Kama Hakuna Wosia wa Marehemu

1.. Mkutano wa ukoo ufanyike kuchagua msimamizi wa mirathi
2. Msimamizi wa mirathi aende kufungua mirathi Mahakamani akiwa na nakala ya uamuzi wa ukoo na cheti cha kifo.
3. Tangazo kutolewa na Mahakama kwa muda wa siku 90. Kama hakuna pingamizi, msimamizi hukabidhiwa barua ya kuhalalisha usimamizi wake.

**WASIMAMIZI WA MIRATHI**

Hawa ni watu ambao wanakuwa wamethibitishwa na mahkama kuwa wasimamizi halali wa mirathi hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 2 ch Sheria ya Mirathi ya Zanzibar.Kazi ya usimamizi wa mirathi ni kazi ambayo inahitaji uaminifu wa hali ya juu. Wanaukoo wawe makini katika kuchagua watu hawa kutokana na madaraka makubwa ambayo sheria inawapa. Uchaguzi mbaya wa msimamizi wa mirathi umeleta madhara makubwa kwenye familia nyingi na mali nyingi imepotea. Hebu tuangalie mamlaka ya msimamizi wa mirathi.

**WAJIBU WA WASIMAMIZI WA MIRATHI**

1. Atakuwa ndio mwakilishi halali wa kisheria wa mambo yote ya marehemu na mali zote za marehemu kisheria zitakuwa chini yake kama msimamizi na sio kwamba ni mali yake,katika kesi ya ***MOHAMED HASSAN v. MAYASA MZEE AND MWANAHAWA MZEE*** [1994] TLR 225 Mahakama ya Rufaani ya Tanzania iliamua kwamba kisheria msimamizi wa mirathi halazimiki kupata ruhusa ya warithi kabla ya kuuza mali yoyote ya marehemu.

Katika kesi ya ***AZIZ DAUDI AZIZ v. AMIN AHMED ALLY&ANOTHER*** CIV. App No.30 of 1990[*unreported*] Mahkama ya Rufaani ya Tanzania at Dar es Salaam iliamua kwamba pale tu msimamizi wa mirathi anapoteuliwa,mali zote zinakuwa chini ya mamlaka yake kama msimamizi na anachukua majukumu ambayo alikuwa nayo marehemu kwenye mali yake wakati yu hai.Msimamizi huyu huachiwa kuamua jinsi ya kushughulikia mirathi hiyo kadri atakavyoona inafaa

2. Atakuwa na mamlaka ya kufungua mashitaka Mahakamani kwa niaba ya marehemu au kushitakiwa kwa niaba ya marehemu na atawajibika kulipa madeni ya marehemu kutoka katika mali alizoacha marehemu.

3.Msimamizi wa mirathi vilevile atakuwa na uwezo wa kuhamisha umiliki wa



mali za marehemu kama atakavyoona inafaa kwa kuziweka rehani, kuziuza au kuzikodisha,kwa kuzingatia maslahi ya warithi na watu wanaomdai marehemu. Hivyo msimamizi wa mirathi hawezi tu kuamka na kutangaza kuuza mali za marehemu bila sababu za msingi.

4. Atawajibika kutumia kiasi fulani cha pesa za marehemu kwa ajili ya kutunza mali za marehemu ziwe katika hali nzuri na zisiharibike.

5. Msimamizi wa mirathi anatakiwa ndani ya miezi sita tangu apewe usimamizi au ndani ya muda mahakama ambao itaona unafaa, anatakiwa apeleke mahakamani na kuonyesha mali zote za marehemu na thamani yake halisi, madeni yake anayodaiwa au anayodai marehemu na ndani ya mwaka mmoja msimamizi wa mirathi atatakiwa tena kama mahakama itakavoona inafaa, aonyeshe mali za marehemu zilizo mikononi mwake na jinsi alivyozifanya au kuzishughulikia.

6.Mahkama ina uwezo wa kuendelea kumuongezea muda muhusika kadri itakavyoona inafaa. Lakini kama msimamizi wa mirathi atatakiwa na mahakama kuonyesha mali za marehemu na akashindwa kufanya hivyo ndani ya muda aliopewa, atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatakiwa alipe faini elfu mbili au apewe kifungo cha miezi sita.

Na kama ataonyesha mali hizo kwa nia ya kudanganya au kuficha atakuwa ametenda kosa la jinai ambalo kifungo chake ni miaka saba.Mtu yeyote mwenye maslahi na mirathi anao uwezo wa kufanya ukaguzi ili kujiridhisha na usimamizi wa mirathi ya marehemu

7.Msimamizi wa mirathi vile vile anatakiwa akusanye mali za marehemu na madeni aliyokuwa akidai na kulipa madeni aliyokuwa akidaiwa,Katika madeni aliyokuwa anadai marehemu ni vizuri msimamizi wa mirathi akayadai mapema ili yasije yakapitwa na wakati kisheria

8. Msimamizi wa mirathi hatakiwi kujipatia faida kutokana na usimamizi wa mirathi hiyo. Msimamizi wa mirathi mwenyewe au kwa kupitia kwa mtu mwingine atanunua mali ya marehemu, uuzaji huo unaweza kukataliwa kisheria na mtu yeyote mwenye maslahi na mirathi hiyo .Moja ya sababu ya kufanya hivyo ni kwamba kuna uwezekano mkubwa akajiuzia mali hizo kwa bei ya chini kuliko thamani halisi ya mali husika.

9. Vile vile ni jukumu la msimamizi wa mirathi kutoa fedha kwa ajili ya shughuli za mazishi ya marehemu,ila gharama hizo ziangalie hali halisi ya maisha ya marehemu na kama ameacha kiasi cha mali cha kutosha kwa ajili ya shughuli hiyo.Kama msimamizi wa mirathi alitoa fedha yake kwa ajili hiyo na haki ya kwanza ya kulipwa fedha zake kabla ya madeni mengine ya marehemu.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA USIMAMIZI WA MIRATHI KWA ZANZIBAR**

Changamoto zinazosababishwa na usimamizi wa mirathi ni;

- Hakuna elimu ya kutosha juu ya kuifahamu sheria ya usimamizi wa mirathi.
- Wengi wa wasimamizi wa mirathi hawatekelezi majukumu yao ipasavyo hivyo kusababisha migogoro katika familia.
- Hakuna uaminifu mara tu mtu anapopewa nafasi ya usimamizi wa mirathi.
- Baadhi ya warithi kukosa haki zao kutokana na chuki baina ya wanandugu.
- Wasimamizi wa mirathi kushindwa kuwajibika inavyotakiwa.

**HITIMISHO**

Ni wajibu kuheshimiwa Sheria za Mirathi ili kuhakikisha mali za marehemu zinagawiwa ipasavyo.



*Meli ya M.V Spice Islander ikiwa imeegesha bandari ya Zanzibar kabla ya kupata ajali ya kuzama*



*Meli ya M.V Spice Islander ikizama katika mkondo mkubwa wa maji ya bahari Nungwi Kaskazini Unguja usiku wa manane Septemba 10,2011 ilipokua ikienda Pemba kutoka Unguja.*



*Baadhi ya maiti iliyoopolewa katika mkondo wa Nungwi ilipozama Meli ya M.V Spice Islander*



*Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein (kushoto) akimueleza jambo Makamo wa kwanza wa Rais Mh. Seif Shariff Hamad walipotembelea Nungwi eneo iliyozama Meli ya M.V Spice Islander*



*Rais wa Tanzania Mh. Jakaya Kikwete (kulia), Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mh. Seif Shariff Hamad (katikati ) na Rais Mstaafu wa Zanzibar Amani Karume wakiwa katika Dua Maalum (hitma) ya kuwaombea waliozama katika Meli ya M.V Spice Islander.*



*Waumin wa Dini ya Kiislamu wakisali sala kuwaombea waliokufa katika Meli ya M.V Spice Islander iliyozama Nungwi*



*Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Maafa Balozi Seif Ali Iddi(kati kati mwenye suti) akijadiliana na wageni waliomtembelea kumpa pole kuhusu ajali ya Meli ya M.V Spice Islander*



*Wanamaji kutoka Afrika ya Kusini walipowasili Uwanja wa Ndege Zanzibar kwa ajili ya kusaidia zoezi la uokoaji wa waliozama katika meli ya M.V. Spice Islander.*



*Rais wa Zanzibar Dk. Ali Shein akimpa pole mmoja kati ya majeruhi ya waliozama katika Meli ya M.V Spice Islander*



*Baadhi ya watu waliokolewa katika ajali ya meli ya M.V Spice Islander iliyozama katika mkondo wa Nungwi.*



*Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Maafa Baloz Seif Ali Iddi akipokea msaada kutoka kwa Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA. Freeman Mbowe kwa ajili ya waliozama katika Meli ya M.V Spice Islander*

# Sheria Inayolinda Zao la Karafuu Zanzibar

**Na Safia Masoud, ZLSC Unguja**

### HISTORIA YA ZAO LA KARAFUU

**ASILI** ya zao hili muhimu ni kutoka kisiwa cha Moluccas huko Indonesia. Zao hili limefika Zanzibar kutoka Mauritius na kuletwa na Waarabu katika mwaka 1818. Mwanzo kabisa ilipandwa katika kasri ya kifalme Mtoni. Zanzibar imepata umaarufu wa uzalishaji wa zao hili ulimwenguni kwa zaidi ya miaka 200 iliyopita. Mwaka 1830 iliongoza kwa uzalishaji na kufikia asilimia 90% katika soko ulimwenguni. Mwaka 1834 ilipata umaarufu zaidi wa zao hili pale ilipozalisha karibu tani 35,000 na kuwa ni nchi pekee kwenye soko la karafuu. Zanzibar iliendelea hivyo kumiliki soko hadi miaka ya 1940 makala hii inaelezea Sheria ya zao la karafuu, Zanzibar.

### SHERIA YA KARAFUU NAM. 11 YA 1985

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kulikuza na kulilinda zao hili ilitunga Sheria Nam. 11 ya mwaka 1985 kwa ajili ya kuweka udhibiti bora wa karafuu Zanzibar. Sheria hii iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 13/06/1985 ina jumla ya Vifungu 12 na imeanza kufanya kazi tokea mwaka 1985.

Kifungu cha 1 kinaeleza kuhusu jina la sheria na kueleza namna ya kufanya kazi kwake.

Kifungu cha 2 kinatoa tafsiri ya maneno yaliyotumika ambayo ni

''Karafuu'' ikiwa na maana ya maua yaliyokauka au vyenginevyo, matende au makonyo

"Shirika" Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kama lilivyoanzishwa na Sheria ya Mashirika ya Umma

''Chombo'' ikiwa na maana ya aina yoyote ya chombo kama dau, mtumbwi, boti ya kuvulia iwe ni ya mashine au la.

''Mamlaka ya Leseni'' maana yake mtumishi wa umma aliyeruhusiwa na sheria yoyote kutoa kibali kwa madhumuni yoyote ambayo inatakiwa na sheria hii.

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na shughuli za karafuu

Kifungu cha 3 (1) kinaeleza kwamba hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kusafirisha nje isipokuwa Shirika.

Kijifungu cha (2) kinaelezea zaidi maana ya kusafirisha ambaye inajumuisha usafirishaji wa karafuu kavu kutoka eneo moja la nchi kwenda eneo jengine bila ya kibali halali kilichotolewa kwa madhumuni ya uchukuaji au usafirishaji ulioelezwa ndani yake

Kijifungu (3) makosa kwa anayekwenda kinyume na Kifungu hiki.

Kifungu cha 4(1) hakuna mtu atakayeruhusiwa kuondosha karafuu mbichi, matende au makonyo kutoka sehemu moja kwenda nyengine isipokuwa kwa kibali halali.

Kifungu cha (2) maelezo ya Kifungu cha (1) hakitumiki kwa kwa wachumaji wa karafuu ambao kwa kawaida wanakuwa wamo katika shughuli za kurudi majumbani kutoka sehemu ambazo ni za uchumaji karafuu.

kijifungu cha (3) mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kijifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Kifungu cha 5 (1) hakuna mtu yeyote atakayesafirisha karafuu au kuvusha karafuu kutoka kisiwa cha Pemba kwa kutumia bandari za Zanzibar. Kifungu cha 2 mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kijifungu atakuwa ametenda kosa.

Kifungu cha 6 (1) (2) kinakataza kwa nahodha au mmiliki wa chombo uchukuzi wa karafuu bila kibali halali kilichotolewa kwa chombo husika na kwa kiwango maalum kilichoruhusiwa na kibali hicho.

Kijifungu cha 6(3) kinaeleza mtu yoyote atakayekwenda kinyume na maelezo ya Kifungu cha 6(1) (2) atakuwa ni mkosa.

Kifungu cha 7 (1) kinaeleza kwamba Shirika la ZSTC ndio linalohusika na ununuzi wa karafuu.

Kijifungu cha (2) kinaeleza kuhifadhi karafuu kwenye nyumba au pahala pengine.

Kijifungu cha (3) masharti ya Kifungu

*Inaendelea Uk. 13*



*Baadhi ya wananchi wakichambua karafuu baada ya kuzichuma Pemba.*





# Sheria Inayolinda Zao la Karafuu Zanzibar

*Inatoka Uk. 12*

hicho cha (2) hayatumika kwa mkulima wa karafuu, mwenye shamba au mkodishwaji wakati wa msimu huu wa uchumaji karafuu.

Kijifungu cha (4) kinaeleza masharti ya kijifungu cha (2) na (3) ya Kifungu cha 7 hayatatumika kwa mtu mwenye kumiliki makonyo katika eneo lake au sehemu nyengine wakati au baada ya msimu wa uvunaji wa karafuu.

Kijifungu cha (5) kinaelezea kwenda kinyume na Kifungu cha 7 atakuwa ametenda kosa.

Kifungu cha 8 (1) kinazungumzia uwezo wa polisi mwenye cheo cha zaidi Msaidizi Mkuu wa Polisi kuruhusiwa kuingia na kukagua maeneo ambayo yanayoshukiwa kuwa masharti ya sheria hii yamekiukwa. Ilimradi afisa huyo wa polisi ana kibali halali cha kufanyia upekuzi.

Kijifungu cha (2) kinafafanua kuwa mtu yeyote atakayemzuia afisa huyo kufanya upekuzi atakuwa amefanya kosa.

Kifungu cha 9 (1) kimelezea adhabu kutokana na makosa yaliopo katika Kifungu cha 3, 5 na 6 na atakayepatikana na hatia atapewa adhabu zifuatazo:-

a) Kifungo kinachozidi miaka 10.
b) Wakati akitumikia kifungo anatakiwa angalau apande miche ya mikarafuu 100 katika eneo litakaloelezwa na waziri.
c) Karafuu pamoja na chombo cha kusafirishia iwe boti, chombo, au dau lililojishughulisha na shughuli hizo kitafilisiwa na Serikali.

Kifungu cha 9 (2) kimeelezea juu ya mtu yeyote ambae atakuwa ni mkosa chini ya Kifungu chengine chochote chini ya sheria hii akipatikana na hatia atapewa adhabu zifuatazo:-

a) Kifungo cha mwaka mmoja,
b) Wakati akitumikia kifungo atapaswa kupanda miche ya mikarafuu isiyozidi hamsini katika eneo ambalo Waziri atalitangaza au
c) Karafuu na chombo kilichotumika kuhifadhia karafuu hizo kitafilisiwa na Serikali

Kifungu cha 10 kinaelezea uwezo wa Waziri wa Fedha kutangaza utozwaji wa ushuru kwa karafuu zote zinazosafirishwa na Shirika.

Kifungu cha 11 kinaeleza uwezo wa Waziri kuandaa kanuni. Ambazo ni:-

a) Kueleza chochote kinachoweza kuelezwa ndani nya sheria hii.
b) kuweka kanuni juu ya ufungaji, kuondoa, kuhifadhi, ukaguzi, usafirishaji wa karafuu zilizonunuliwa kutoka katika Shirika.
c) Kuweka kanuni ya matumizi ya majahazi, mitumbwi pamoja na vyombo vyengine vya usafirishaji karafuu na ukaguzi wa karafuu kabla, wakati na baada ya usafirishaji.
d) Kuweka utaratibu kwa aliyetiwa hatiani juu na namna ya kupanda miche ya mikarafuu.

Kifungu cha 12 (1) kinafuta Sheria ya karafuu Nam. 8 ya mwaka 1970.

Kwa ujumla sheria inazungumzia juu ya taratibu za uuzaji, usafirishaji pamoja na taasisi husika inayohusika na ununuzi wa karafuu ambalo ni Shirika la ZSTC.



*Mti wa Mkarafuu*



*Baadhi ya wananchi wakiwa katika Kituo cha uuzaji wa karafuu, Pemba.*

### KANUNI ZA SHERIA YA ZAO LA KARAFUU

Sheria hii ina kanuni zake mbili ambazo zote zimeanza kufanya kazi kuanzia tarehe 1 Julai 2002.

1) Kanuni hii pamoja na mambo mengine inazungumzia masuala yafuatayo:-
   - Namna ya utoaji vibali na anayehusika kutoa kibali ambaye ni sheha wa shehia husika;
   - Uthibitishaji wa kibali cha chombo cha usafirishaji ambaye ni Mkuu wa Wilaya au Afisa atakayeruhusiwa na Mkuu wa Wilaya
   - Kusajili mashamba ya karafuu;
   - Kukodisha mashamba ya karafuu;
   - Uwekaji wa kumbukumbu za mauzo kwa muuzaji, kumbukumbu zitakazowekwa na Shirika;
   - Ukaguzi wa karafuu ambao unaweza kufanywa na polisi au sheha kwa ajili ya kuangalia karafuu zilizohifadhiwa wakati wa msimu wa uvunaji na kuweka kumbukumbu pamoja na taratibu nyengine;
2) Kanuni hii inazungumzia msimu wa uvunaji karafuu ambayo ni misimu miwili. Msimu wa mwaka ambao unaanzia 1 Julai mpaka mwisho wa Novemba kwa kila mwaka. Msimu wa pili ni vuli.

### HITIMISHO

Sheria hii pamoja na kanuni zake zimetungwa muda mrefu. Hivyo kutokana na mabadiliko ya wakati hasa katika nyanja za uchumi, ni vyema sheria hii ikaangaliwa upya ili iweze kufanyiwa marekebisho kwa kutoa fursa zaidi kwa wananchi kushiriki katika kulizalisha zao hili pamoja na kuangalia nyanja nyengine ambazo zitaweza kuzalishwa kutokana na zao hili ili wananchi wapate soko la kuuza bidhaa mbalimbali zinazotokana na zao hilo.

# Ijue Haki ya Kusikilizwa *(Audi Alteram Parterm)*

Na Siti H. Moh'd, ZLSC Pemba

**UTANGULIZI:**

**HAKI** ya kuskilizwa ni haki ya msingi ya kimaumbile ya binadamu (*natural justice*). Haki hii ni muhimu kupewa kwa kila mtuhimiwa/mshtakiwa kabla ya kutolewa maamuzi ya kesi yake inayomkabili. Mahkama inasisitiza umuhimu wa haki ya kusikilizwa kutekelezwa. Haki hii imeelezwa katika Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948 na katika Katiba za nchi. Sura ya tatu, Kifungu cha 12(6)(a) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 kinaeleza kwamba:-

*"Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa Mahakama au chombo kinginecho kinachohusika basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia kukata rufaa au ya kupata kitulizo kinginecho cha kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika"*

Pia haki hii imeelezwa katika Ibara ya 13(6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka wa 1977

**DHANA YA HAKI YA KUSIKILIZWA:**

Haki ya kusikilizwa ni ya msingi na lazima kupewa kila mshtakiwa/mtuhumiwa. Pande zote mbili katika kesi zinalazimika kupewa fursa ya kusikilizwa kabla ya kutolewa maamuzi. Hakuna uamuzi utakaokuwa ambao utakuwa sahihi ikiwa pande husika katika kesi hazitopewa nafasi ya kusikilizwa. Katika kesi ya ***PAINTER v.LIVERPOOL OIL GAS LIGHT CO.*** (1836) A&E 433, imeelezwa kwamba "*hakuna upande wowote ule utakaosumbuliwa na mtu bila ya kuwa na haki/fursa ya kusikilizwa*" (*a party is not to suffer in person without an opportunity of being heard.*)

Kabla ya hukumu kutolewa kwa mtu yoyote, fursa ya kusikilizwa ni lazima apatiwe mtu huyo. Ili haki hii ikamilike mambo mawili makuu ni vizuri yazingatiwe. Mambo yenyewe ni kama yafuatayo:-



***Askari Polisi akijaribu kumtuliza mtuhumiwa***

1. Taarifa (*notice*).
2. (2) Kusikilizwa (*hearing*).

**TAARIFA (*NOTICE*)**

Ni lazima upande wa utetezi katika kesi kupewa taarifa ili kuonesha chanzo au asili ya tatizo liliopo dhidi yake kwa ajili ya kutoa maelezo (kujitetea). Hukumu au uamuzi wowote utakaotolewa bila ya kutolewa taarifa kwa upande husika uamuzi huo utakiuka dhana ya haki za msingi za kimaumbile (*natural justice*) na uamuzi huo utakuwa ni batili.

Katika kesi ya ***R v. UNIVERSITY OF CAMBRIDGE*** (1723) 1 Str 757:93 ER 698 imeelezwa kwamba kwa kuwa haki ya kupewa taarifa haikutolewa, Mahkama iliyakataa maamuzi na kusema sio halali na ni batili.

**DHUMUNI LA UPEWAJI WA TAARIFA**

Kuna umuhimu mkubwa wa utoaji wa taarifa kwa mshtakiwa/mtuhumiwa, ambapo ni pamoja na:

- Kutoa fursa kwa muhusika kuweza kujua kilichomkabili dhidi yake.
- Kujiweka tayari kwa ajili ya kusikilizwa na kutoa maelezo ya utetezi wake.

*Inaendelea Uk. 15*





# Ijue Haki ya Kusikilizwa *(Audi Alteram Parterm)*

*Inatoka Uk. 14*

Kwa hivyo pale ambapo taarifa iliyotolewa inaendana na kosa moja tu, mtu huyo hatoadhibiwa/hatohukumiwa kwa kosa jengine tofauti ambalo hajapatiwa taarifa inayohusiana na kesi hiyo kama ilivyoelezewa katika kesi ya ***ANNAMUNTHOLO V. OILFIELD WORKERS*** (1961) 3ALLER 621

- **HAKI YA KUSIKILIZWA**

Kupewa haki ya kusikilizwa ni miongoni mwa chanzo kikuu kinachopelekea upatikanaji wa haki kwa mshtakiwa/ mtuhumiwa kwasababu ya kujitetea kwake kutokana na kesi inayomkabili dhidi yake, haki hii anatakiwa apewe kabla ya kutolewa uamuzi wa kesi hiyo.

Mfano wa kesi ambayo haikutolewa haki ya kusikilizwa na maamuzi yake hayakuzingatiliwa ni:- ***COOPER v. WANDSOWRTH BOARD OF WORKS*** (1863) 14 CB: Mdaiwa ilikuwa ni Bodi iliyovunja nyumba ya mdai bila ya kutoa haki ya kusikilizwa kwa mdai. Mahakama iliamua kwamba uwezo wa Bodi ulitawaliwa na sifa ambazo hakuna mtu yoyote atakayenyang'anya haki ya mwenzake bila ya kutoa haki ya kusikilizwa.

Vile vile haki ya kusikilizwa inaonekana katika kesi ya ***MASUMBUKO RASHID***.v. R [1986] TLR 72 ambapo mkata rufaa na wenzake watatu walishtakiwa kwa kosa la wizi wa kutumia nguvu na kukutwa na silaha ya moto. Washtakiwa walitiwa hatiani bila ya kupewa haki ya kusikilizwa. Washtakiwa walikata rufaa katika Mahkama Kuu Tabora na Jaji Chipeta aliamua kwamba Mahakama ya Mkoa iliwahukumu washtakiwa bila ya kupewa haki ya kusikilizwa nailivunja msingi ya haki za kimaumbile.

Katika kesi ya ***SADIKI ATHUMANI v. R*** [1985] TLR 5. mkata rufaa pamoja na mwenzake walishtakiwa kwa kosa la wizi wa ng'ombe. Walikata rufaa Mahkama Kuu, Dodoma, Jaji SAMATA alitoa uamuzi



***Askari wa kutuliza Fujo (FFU) wakimkabili mtuhumiwa.***

ambao unapingana na uamuzi wa Mahkama ya Wilaya kwa sababu Mahkama ya Wilaya haikutoa haki ya kusikilizwa kwa washtakiwa hawa.

Kuna baadhi ya kesi ambazo pande zote mbili zinakuwepo mbele ya Mahkama lakini wanakuwa wanaekewa vikwazo katika kutoa maelezo yao kuhusiana na kesi hiyo iliyowakabili na hivyo kupelekea kesi hiyo kutolewa maamuzi bila ya kupewa haki ya kusikilizwa kwa pande mbili hizo. Hivyo basi haki ya kusikilizwa ni lazima itolewe bila ya kuekewa vikwazo vyovyote vile ili iweze kuleta tija juu ya kesi inayobishaniwa na kupelekea kutolewa maamuzi yaliyo sahihi na ya haki baina ya pande mbili hizo.

Kutokana na maelezo hayo hapo juu Mamlaka husika ambazo zinatoa haki ni lazima ziangaliye kwa makini dhana ya maadili ya haki za kimaumbile.

- Haki ya kusikilizwa kwa kutoa maelezo ya mdomo.

Mtuhumiwa/mshtakiwa hafungamani na kusikilizwa kwa maneno ya mdomo tu isipokuwa iwe haki hiyo imeidhinishwa na sheria.

Katika kesi ya ***M.P. INDUSTRIES v. UNION OF INDIA*** (1966) SC 671: Subba Rao, J ameeleza kwamba

*"Hakuna shaka juu ya dhana ya maadili ya haki za asili za kimaumbile kwamba si maamuzi ya mahakama wala taasisi za mahakama haziwezi kutoa maamuzi yoyote kwa upande husika bila ya kutoa fursa ya kuekewa mkutano kuhusiana na shtaka linalomkabili dhidi yake lakini haki hiyo si lazima iwe ni ya kumsikiliza mtu mwenyewe.*

*Maelezo ya maandishi au kumsikiliza mtu mwenyewe itategemea aina ya jambo linalobishaniwa na kwa kawaida inakuwa ni uwezo wa Mahakama.*

*Dhana ya madili ya haki za kimaumbile haihitaji kumsikiliza mtu mwenyewe na hasa ikiwa mazingira yote yanayoendana na kesi yametiliwa manani kabla ya kuchukuwa hatua zozote zenye kutia mashaka".*

**HITIMISHO**

Taasisi zote zinazohusika na utoaji wa maamuzi zinapaswa kuizingatia haki hii kabla ya kutoa maamuzi yoyote dhidi ya mtu aliye na kesi mbele yake. Pia jamii inapaswa izingatie haki hii ya msingi zaidi kwa watoto wao kwa kutotoa maamuzi na kujichukulia hatua bila ya kuwasikiliza.

# Sheria Zinazolinda Haki za Mwanamke

Na Harusi Mpatani, ZLSC Unguja

**UTANGULIZI**

**HISTORIA** inatuonesha kwamba wanawake ni miongoni mwa makundi yanayodhalilishwa na kukoseshwa haki zao za msingi ambazo kila binadamu ana haki kuzipata. Tamaduni, mila na desturi vilitumika kuwafanya wanawake wayakubali mazingira ya kunyanyaswa, kudhalilishwa na kutokuwepo uwiano katika jamii zao. Mtoto wa kike ananyimwa fursa nyingi muhimu kutokana na mgawanyo wa kazi na majukumu katika jamii inayomzunguka ikiwemo haki ya kupata elimu, haki ya kushiriki katika mambo ya kisiasa, kiuchumi na hata mambo ya kushauriana ndani ya jamii ikiwa yeye ni mmoja ya wanajamii wenyewe, na badala yake alibebeshwa majukumu ya kazi za nyumbani. Ni wajibu jamii kubadilika na kuheshimu sheria ili wanawake wapate haki zao.

**HISTORIA FUPI YA MWANAMKE KUKOMBOKA KISHERIA**

Baada ya vita vikuu vya pili vya Dunia mwaka 1945 mataifa makubwa yalikutana na kutafakari kwa kina ukatili na uvunjwaji wa haki za binadamu ulivyokuwa umekithiri katika vita hivyo. Wanawake na watoto waliathirika sana. Mataifa hayo kwa kauli moja yaliungana na kujulikana Jumuiya ya Madola**.** Azma kubwa ilikuwa ni kukomesha vitendo vyote vya ukatili, ubaguzi pamoja na unyanyasaji dhidi ya mwanamke na walitoa Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948. Ibara ya (1) ya Tamko hilo linasema:

*"Binadamu wote huzaliwa wakiwa huru na sawa katika utu na haki zao."*

Ibara hii ndio msingi wa harakati za ukombozi wa haki za binadamu na kuwa chachu ya wanawake kudai haki zao. Mnamo mwaka 1979 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW). Mkataba huu umeanza kutumika rasmi kama mkataba wa kimataifa mnamo mwaka 1981 baada ya nchi zisizopungua 80 na kuridhia mkataba huo na kufikia nchi 187 kati ya nchi 193 kuuridhia hadi kufikia mwaka 2011.

**BARA LA AFRIKA**

Utekelezaji wa haki za binadamu katika bara la Afrika ulipata msukumo mkubwa baada ya kuanzishwa kwa Mkataba wa Haki za Binadamu mwaka 1981. Utanguliza wa mkataba huo unasema:

*"Uhuru, usawa, haki na utu ni vitu vya lazima katika kufikia matarajio halali ya watu wa Afrika"*



**TANZANIA NA HAKI ZA WANAWAKE**

Kupitishwa kwa Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake kumepelekea nchi nyingi ulimwenguni zilizoridhia Mkataba huu kufanya marekebisho makubwa katika Sheria zao za ndani ili kwenda sambamba na malengo ya mkataba huo. Tanzania ikijumuisha Zanzibar iliridhia mkataba huo.

**SHERIA ZA ZANZIBAR NA HAKI ZA WANAWAKE**

Takriban haki zote zilizoelezwa katika Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Mwanamke zinatambuliwa na kulindwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sheria nyengine mbalimbali kwa mfano kuna mabadiliko makubwa katika sheria ya Ajira ya Zanzibar Nam.5 ya 2005 ambayo sasa inampa haki na fursa sawa muajiriwa mwanamke.

**KATIBA YA ZANZIBAR YA MWAKA 1984**

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeelezea haki ya usawa katika Kifungu cha 11(1) cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza ''*binadamu wote huzaliwa huru"* . Aidha kifungu cha 11(2) cha katiba kinaeleza kuwa; ''*kila mtu anastahiki heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake"* na haki ya usawa mbele ya sheria kuwa watu wote watakuwa sawa mbele ya sheria na wanayo haki sawa mbele ya sheria bila ya kubagua jinsia, dini, rangi na asili ya mtu. Zifuatazo ni baadhi ya sheria zinazomlinda mwanamke zanzibar

**SHERIA YA ADHABU NAM. 6 YA 2004.**

Sehemu ya **XV** ya Sheria hii inazungumzia makosa mbalimbali kuhusiana na makosa kinyume na maadili *(Offences against morality)*

Kifungu cha **125 (1)** kinasema; ni kosa la jinai kwa mwanamme kumbaka mtoto wa kike au mwanammke. Pia katika kijifungu kidogo cha **(2)** kinaelezea jinsi gani mwanamme atasemekana amefanya kosa la kubaka, kwa kusema kuwa mtu atahesabiwa kuwa amefanya kosa la kubaka iwapo atafanya tendo la ndoa na msichana ambaye yupo chini ya umri wa miaka 18 iwe kwa hiari au kwa kulazimishwa.

Kifungu cha **125 (3)** kimebainisha kuwa mtu ambaye anawadhifa katika mamlaka fulani akatumia wadhifa huo kwa kufanya kitendo cha ubakaji kwa msichana au mwanamke kutokana na mahusiano ya kikazi au kumuweka kizuizini isivyo halali na kufanya kosa la ubakaji kwa msichana au mwanamke huyo.

Jambo jengine lililozungumziwa ndani ya Sheria hii kwa kumlinda mwanamke ni shambulio la aibu ambalo limezungumziwa katika Kifungu cha **131 (1)** pamoja na udhalilishwaji wa kijinsia unaoelezwa katika Kifungu cha **158** cha Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya 2004 kuwa ni kosa kutoa neno lolote ambalo litatumika, sauti yenye ishara au kitu chochote kwa azma ya kumaanisha neno Fulani ambapo itapelekea kuondoa staha kwa mtu huyo.

Sheria hii imetoa adhabu kwa mtu aliyefanya kosa la kubaka kwamba kifungo, faini pamoja na kuipa mahakama uwezo wa kumuamuru mtuhumiwa kumlipa muathirika fidia kwa athari zote alizomsababishia zikiwemo za mwili na kiakili.

**SHERIA YA ELIMU NAM. 6 YA 1982.**

Elimu ni moja ya haki muhimu kwa kila mtoto bila ya kubaguliwa, akiwa mwanamme au mwanammke ili kuweza kujiendeleza kimaisha.

Haki hii imeelezwa katika Kifungu cha **19** cha **Sheria ya Elimu Nam. 6/1982** kwa kusema kuwa

*Inaendelea Uk. 15*





# Sheria Zinazolinda Haki za Mwanamke

*Inatoka Uk. 16*

*" Itakuwa ni lazima kwa kila mtoto aliyefikia umri wa miaka saba lakini hajazidi kumi na tatu kuandikishwa Elimu za msingi"*

Kifungu hiki kinamaanisha kwamba haki ya elimu ni haki ya jamii nzima bila ya kujali tofauti ya kijinsia hivyo pale fursa hiyo itakapokosekana ni wajibu wa mtu kuidai ili kuweza kufanikisha maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Vile vile, Kifungu cha 20 (1) kimeweka wazi wajibu wa mzazi au mlezi wa kila mtoto alieandikishwa katika elimu ya msingi kwamba analazimika kuhakikisha kuwa anahudhuria skuli hadi anamaliza elimu hiyo ya msingi (ikijumuisha pamoja na Elimu ya Sekondari ya Awali ambayo kila mtoto wa Zanzibar ni wajibu kuipata.). Na katika Kifungu kidogo cha (3) cha Kifungu hiki kimeeleza kuwa hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa kabla hajamaliza Elimu ya Msingi pamoja na Sekondari ya Awali.

Kifungu cha 34 cha Sheria hii kimesema kwamba mtu yoyote ambaye atakwenda kinyume na Kifungu cha 20 cha Sheria hii atakuwa amefanya kosa na atapewa adhabu kama zilivyoainishwa katika sheria hii. Mbali na vifungu hivyo, lakini pia Kifungu cha 20 (4) ambacho hapo awali kilikuwa kinamnyima fursa mtoto wa kike kuendelea na masomo pindi atakapobainika kuwa amebeba mimba kimefutwa na Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa mzazi mmoja Sheria Nam. 4 ya 2005. ambapo Sheria hiyo imetowa fursa kwa mwanafunzi ambaye atapata mimba kuendelea masomo yake mara tu baada ya kujifunguwa na kutimiza masharti yaliyowekwa na sheria hiyo.

**SHERIA YA KUWALINDA WARI NA WATOTO WA MZAZI MMOJA NAM. 4 YA 2005**

Kabla ya kufanyiwa marekebisho sheria hii, Sheria ya awali yaani Sheria ya kuwalinda wari, na wajane Nam. 4 ya 1985 ilikuwa imesema kwamba ni kosa kwa mtoto wa kike mwari kupata mimba kabla hajaolewa na adhabu yake ilikuwa ni kifungo cha miaka miwili jela, Sheria hii iliwaathiri sana watoto waliokuwa na umri kati ya miaka 17 – 18. Hivyo, mara baada ya kupitishwa Sheria Nam. 7 ya 1998 ilipelekea kubadilishwa kwa kosa hilo na kuweka kuwa msichana aliye katika umri huo hata akipata mimba kwa hiari yake atahisabika kuwa amebakwa, kwahiyo haitowezekana kushtakiwa kwa kosa la kupata ujauzito. Sheria hii pia ilirekebisha umri wa mwari na kuweka kuwa miaka 18 - 21 badala ya ule wa 16 –25 na kuweka kuwa bado ni kosa kwa mwari kupata mimba nje ya ndoa hata ikiwa kwa hiari yake, na kubadilishwa adhabu yake kuwa kutumikia vituo vya jamii kwa muda wa miezi 6 badala ya kifungo.

Pamoja na hayo, pia Sheria hii imejaribu kuwatizama watoto ambao huzaliwa nje ya ndoa (mzazi mmoja) ambao huwa mzigo kwa upande wa mama pekee katika kulea na kumpatia huduma muhimu za matunzo ya mtoto huyo ikiwemo chakula, mavazi, matibabu,, elimu n.k. Kutokana na kuundwa kwa Sheria hii majukumu hayo yamepunguzwa kwa mama na kupewa baba wa mtoto na kumpa haki mama wa mtoto huyo kudai huduma za matunzo hayo kisheria kwa baba mtoto ikiwa baba huyo hatoyatimiza majukumu hayo. Haki hiyo ya kudai kisheria amepewa mama huyo wakati wowote kuanzia ndani ya uja uzito huo hadi mtoto aliyezaliwa atimize umri wa miaka 18.

**SHERIA YA AJIRA NAM. 11 YA 2005**

Sheria ya Ajira ni miongoni mwa sheria zinazofuata katiba pamoja na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu. Sheria hii imekataza ubaguzi miongoni mwa wafanyakazi kutokana na jinsia zao, kwahiyo mfanyakazi yoyote awe mwanamme au mwanmke anahaki ya kupata fursa sawa bila ya kujali tofauti za kimaumbile baina yao.

Kifungu cha 10 cha Sheria hii kimeainisha kwamba ni marufuku kwa muajiri kumbagua mfanyakazi kwa kigezo cha kabila, jinsia, rangi, dini, cheo, umri, sehemu aliyotoka, mtazamo wake kisiasa, ulemavu,kuathirika kwa maradhi ya ukimwi n.k. vilevile Kifungu kidogo cha (2) cha Kifungu hicho kinaeleza kwamba muajiri analazimika kuchukuwa hatua:

(a) Kutoa fursa sawa katika sehemu ya kazi na kuondoa ubaguzi katika sera yake na utendaji wake.
(b) Kuthibitisha kuwepo kwa malipo sawa ya mishahara kwa mwanamke na mwanamme kwa kazi ya aina moja.

Suala jengine lililokatazwa na kukemewa katika Kifungu cha 11 cha Sheria hii ni unyanyaswaji wa kijinsia, vitendo vya kumtaka muajiriwa wa kike kimapenzi, vitisho na lugha inayoashiria mapenzi ( ngono) .

Sababu moja ya waajiri wengi kukataa kuwaajiri wafanyakazi wanawake ni kuwa muda mwingi watakuwa hawapo kazini kutokana na kujifungua. Suala ambalo limekatazwa moja kwa moja na Sheria hii.

Katika kuhakikisha ya kwamba mwanamke anapata nafasi nzuri ya mapumziko na kulea mtoto wake vizuri, Sheria ya Ajira pamoja na kanuni za Utumishi Serikalini zinatoa haki ya kupata likizo ya uzazi kwa muda wa miezi mitatu baada ya kujifungua na mfanyakazi atapata likizo hii kila baada ya miaka mitatu ambayo haitaingiliana na likizo yake ya kawaida. Kifungu cha 70 (1) cha Sheria hii kinaelezwa kwamba

*"mfanyakazi mwanamme ambae ni mjamzito mara baada ya kujifunguwa anastahiki likizo ya miezi 3 yenye malipo ambayo haihusiani na likizo yake ya kawaida ya kila mwaka "*

Na ikiwa muajiriwa huyo atajifunguwa mapacha basi atapata likizo ya siku mia moja Kifungu cha 70 (2). Baada ya likizo ya uzazi kumalizika muajiriwa huyo atakuwa na haki ya kupewa muda wa saa moja katika muda wakazi kwenda kunyonyesha (Kifungu cha 70 (a) ) cha Sheria hii.

Kwa ujumla sheria hii imemuekea mazingira ya usalama mfanyakazi mwanamke kwa kutoa masharti kadhaa kwa muajiri. Kifungu cha 84 na 85 vya sheria hii vinathibitisha hayo; mfanyakazi mwanamke ambaye ameajiriwa au amepangiwa kufanya kazi ya kunyanyua vitu vizito, inatakiwa muajiri ahakikishe kuwa uzito atakaopewa kunyanyua mwanamke usizidi nusu ya ule atakaonyanyua mwanamme .

Aidha ni marufuku kumuajiri mwanamke katika sehemu ambazo zinahusika na kemikali za sumu ambazo zitahatarisha uzazi au mimba ya mfanyakazi huyo kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 84 (4)

Kifungu cha 85 (1) kinaeleza kwamba ni kosa kumuajiri, kumpangia kazi mfanyakazi mwanamke wakati wa usiku katika shughuli zozote za viwanda isipokuwsa tu zile zilizoruhusiwa na Sheria hii kama ilivyoelezwa katika Kifungu 86 cha Sheria hii

**CHANGAMOTO**

Ingawa kuna sheria nyingi zinazomlinda mwanamke Duniani, Tanzania na Zanzibar kwa ujumla lakini bado kuna unyanyasaji mwingi wa wanawake, hii inatokana na baadhi ya watu kutotaka kuzifuata sheria zilizopo na uwelewa duni wa sheria zinazomlinda mwanamke.

**HITIMISHO**

Nafasi ya mwanamke katika ulimwengu huu ni kubwa na muhimu ambapo anachukua asilimia 52 ya watu wote duniani, Hivyo basi mwanamke anahitaji kutunzwa na kuendelezwa kielimu pamoja na kupatiwa haki yake kama binadamu ili kusiwe na jamii ambayo haina muelekeo.



Mhadhiri wa Sheria Chuo Kikuu, Tunguu Zanzibar, Ali Uki akichangia katika Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.


Mshiriki wa Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano, akitoa mawazo yake kuhusu Muungano wa Tanzania katika Mdahalo wa Katiba mpya uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.


Mkalimani wa lugha ya ishara akitafsiri kwa watu wasioweza kusikia katika Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano, katika Katiba mpya uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.


Mshiriki wa Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano, Juma Said Sanani akitoa mawazo yake kuhusu Muungano wa Tanzania katika Mdahalo wa Katiba mpya uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.


Mshiriki wa Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano, Mwamvua Mfaume akitoa mchango wake katika Mdahalo wa Katiba mpya uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.


Mshiriki wa Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano, Hussein Ibrahim akionesha waraka kujenga hoja kuhusu Muungano wa Tanzania katika Mdahalo wa Katiba mpya uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.

## Lazima Wawajibishwe Wote Walomakosani

Awali Naazilia, yaliyo mwangu moyoni
Huku nikijinamia, moyo uko tafrani,
Kila nikikumbukia, yaliyojiri nchini
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Nchi imejinamia, huzuni tele nyoyoni
Ajali kutufikia, humu kwetu visiwani
Meli ilojizamia, huko nungwi mkondoni
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Vifo vingi metokea, jamaa na wahisani
Watoto watu wazima, wakike na kiumeni
Ajali mewafikia, mbaya isiyo mithali
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Sababu naeelezea, uzembe uloshamiri
Kwa abiria kujazwa, ovyo humo kwenye meli
Bila hata kuchunguzwa, chombo kiko hali gani
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Na mizigo kadhalika, mingi iliyosheheni
Bila kiwango kuekwa, napia bila idadi
Mingi imekizidia, chombo hicho baharini
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Mamia walojifia, watoto wamo kundini
Nini walichokosea, hata kuwa mashakani
Haki iloondolewa, ya kuishi duniani
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Haki iliyo muhimu, kila mtu duniani
Na katiba yalazimu, kwa kutuweka mwangani
Ni kosa kuzidhulumu, nafsi zetu yakini
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Pia tunawapongeza, hawa wetu viongozi
Msada kuharakisha, kuokoa baharini
Wote yaliyowakuta, maafa haya majini
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

Jitihada za haraka, kwa kuleta waokozi
Taasisi zote umma, wote tuko ufukweni
kunusuru kwa haraka, maisha yalokabili
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

pia na kuundwa tume, ukweli kuutambau
wakosa wawajibishwe, kwa kila alochangia
sheria mkondo wake, vyema kufuatilia
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani**

kwa kufika ukingoni, dua tunawaombea
uwaingize peponi, walokwisha tangulia
uwape swiha mwilini, wale waliobakia
**Lazima wawajibishwe, wote walo makosani.**

**Jina Mwinyi Waziri,**
**ZLSC,**
**Unguja.**





# Sheria Mpya Zanzibar


*Jengo la Baraza la Wawakilishi*

**BARAZA** la Wawakilishi la Zanzibar limejadili na kupitisha jumla ya sheria saba kuanzia Januari hadi Oktoba, 2011. Sheria hizo zimeshasainiwa na Rais wa Zanzibar.

Aidha, Baraza la Wawakilishi limejadili na kupitisha Miswada mitatu ambayo haijasainiwa na Rais; hivyo bado ni Miswada. Kwa mujibu wa Kifungu cha 63 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinasema kwamba *"…..basi jambo halitakuwa na nguvu za kisheria mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vile vile na Rais".*

Kifungu cha 63 (2) kisomeke pamoja na Kifungu cha 78 (2) kinachosema kwamba *"bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, nguvu za kutunga sheria katika Baraza la Wawakilishi itakuwa kwa kupitishwa Miswada katika Baraza la Wawakilishi".*

Vile vile, Kifungu cha 78 (3) kinasema kwamba *"wakati Mswada umepitishwa na Baraza la Wawakilishi, Spika ataupeleka kwa Rais ndani ya siku thelathini kupata kibali chake".*

Aidha, Kifungu 79 (1) kinasema kwamba "….*Rais anaweza ndani ya siku tisini ama kukubali au kukataa kuukubali, na iwapo atakataa Mswada, basi ataurudisha kwenye Baraza la Wawakilishi pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali Mswada huo."*

Vile vile, Kifungu cha 79 (2) kinasema kwamba *"…..baada ya siku tisini tokea siku ya kuwasilishwa mswada kwa Rais kumalizika bila ya kukubaliwa au kukataliwa na Rais, Mswada huo utachukuliwa kuwa ni Sheria".*

**SHERIA**

1. Sheria ya kuweka masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma Zinazolingana na Hizo – Nam. 1/2011.
2. Sheria za Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar – Nam. 2/2011.
3. Sheria ya Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6/2001 na Kuweka Sheria Mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu – Nam. 3/2011.
4. Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika Nam. 4/2011.
5. Sheria ya Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA) Nam. 3/1988 na Kutunga Sheria Mpya ya Uhakiki wa Chakula na Lishe, Zanzibar – Nam. 5/2011.
6. Sheria ya Mtoto itakayotoa Haki na Maslahi Bora ya Mtoto, Itakayoshughulikia Watoto na Matatizo na Sheria, Ulezi, Ukaaji, Kumuona na Kumtunza Mtoto, Kuwasili, Hatua maalum za Kiunga Kuhusiana na Mtoto, Ridhaa ya Utabibu wa Kidaktari, Itakayoanzishwa Skuli za marekebisho, Makaazi na Matunzo ya Kutwa itakayorekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Kusahihisha Sheria Zinazohusiana na Mambo Haya – Nam. 6/2011.
7. Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Kazi zake na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo – Nam. 8/2011.
8. Sheria ya Kuweka Masharti ya Utawala, Udhibiti na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar – Nam. 9/2011.

**MISWADA**

1. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.
2. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo.
3. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha baadhi ya Sheria na kuweka masharti bora ndani yake.

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI
Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki
Iwe shauku

Toleo Na. 007 | Jarida la kila miezi mitatu | Julai - Septemba, 2011

# Sauti za Wananchi Zipewe Nafasi Katika Katiba Mpya

**WASHIRIKI** wa Mdahalo wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamesisitiza umuhimu wa wananchi kushirikishwa kujadili aina ya Katiba wanayoitaka.

Walisema ushirikishwaji wa umma katika utayarishwaji wa Katiba mpya ni nguzo muhimu ya demokrasia na kutawafanya wananchi kuiheshimu na kuhisi ni Katiba yao.

Washiriki wa Mdahalo huo wa wazi walikuwa wakijadili mada *"Mustakbali wa Muungano katika Katiba Mpya"* iliyowasilishwa na Mwanasheria Mwandamizi Zanzibar, Ibrahim Mzee Ibrahim, katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

Walisema kwamba wananchi wa pande zote mbili za Muungano hawakushirikishwa katika utayarishaji wa Katiba zote tano za Tanzania na Katiba tatu za Zanzibar.

"Wananchi walinyimwa haki ya kutoa mawazo yao na kujadili Katiba zao," walisema na kusisitiza kwamba sauti za wananchi lazima zipewe uzito katika Katiba mpya.

Aidha, washiriki walisema ni kinyume na demokrasia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupewa mamlaka ya kutayarisha hadidu rejea *(terms of reference)* peke yake bila ya kuwashirikisha wananchi.

Walisema kwamba Rais anaweza kutayarisha hadidu rejea ambazo zitakuwa na ushawishi wa mjadala kulenga matakwa anayotaka yeye binafsi.

Vile vile, hoja mbali mbali za kuboresha kasoro za kikatiba na kiutawala zinazoleta kero katika Muungano zijadiliwe kwa uwazi na kutafutiwa ufumbuzi unaofaa.

Mdahalo huo uliokuwa ukitangazwa moja kwa moja katika baadhi ya redio na televisheni ulitayarishwa kwa mashirikiano bainya ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kiliopo Kijitonyama, Dar es Salaam.



*Mwanasheria Ibrahim Mzee Ibrahim akiwasilisha mada ya Mustakbal wa Muungano katika Katiba mpya, katika mdahalo wa Katiba uliofanyika SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.*



*Mwanasheria Harold Sungusia kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Dar es Salaam akitoa maelezo mafupi kabla ya ufunguzi wa Mdahalo wa Katiba uliofanyika SUZA Zanzibar.*



*Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society) Stola akichangia katika Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.*



*Baadhi ya washiriki wa Mdahalo wa Mustakbali wa Muungano SUZA Septemba mwaka huu Zanzibar.*